

# Ushirikiano Wa Nishati Endelevu Ya Nguvu Za Maji Kidakio Cha Kiwira

## Lengo: Kuweka misingi sawia na endelevu ya matumizi ya maji kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Kidakio cha Kiwira

| | |
|---|---|
| **Jina la Ushirikiano** | **Ushirikiano kwa ajili ya nishati endelevu ya nguvu za Maji katika Kidakio cha Kiwira** |
| **Awamu ya kwanza** | Februari 2018 – Disemba 2018 |
| **Washirika** | Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa |
| | Kiwira Energy Ltd. /Frontier investment |
| | Halmashauri ya Wilaya ya Ileje |
| | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe |
| | Ensol Tanzania Ltd./Bwelui Ltd |
| | Kikundi cha Mazingira Ileje Mashariki (KMIM) |
| | GIZ Water Bilateral Program |
| | GIZ Energy Programme |
| | International Water Stewardship Programme (IWaSP) |



Wadau wakiwa katika hatua za maandalizi ya ushirikiano, Kiwira 2, August 2017

### *Muktadha*

Kidakio cha Kiwira chenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,900 kipo Mkoani Mbeya, Tanzania katika Bonde la Ziwa Nyasa. Eneo la Kidakio hiki linakadiriwa kuwa na takribani watu 300,000 (Makadirio 2017). Likipata mvua kwa mwaka kiasi cha mm 1,866 na wastani wa mtiririko wa maji kiasi cha mm 935 kwa mwak. Eneo hili linachangia 12% ya maji yote yatiririkayo kwenda Ziwa Nyasa.

Ili kufanikisha malengo ya ushirikano huu, washirika, taasisi husika za serikali pamoja na jamii katika kidakio cha kiwira watafanya kazi pamoja katika maeneo makuu sita (6):

1. Kukusanya na kusambaza taarifa na data
2. Usimamizi wa maji
3. Ushirikishwaji wa wadau na mipango shirikishi
4. Uhifadhi wa kidakio
5. Maendeleo ya nishati ya nguvu za maji na
6. Uratibu wa ushirikiano

| **Ushirikiano huu umegawanywa katika shirikiano mbili ndogo** | |
|---|---|
| **Ushirikiano wa Kiwira Juu-Kati** | Kampuni ya Kiwira Energy Ltd inalenga kuendeleza miradi miwili ya nishati ya nguvu za maji katika eneo hili. Inategemewa kuwa kati ya 1.6 na 6.9MW zitazalishwa.<br><br>Awamu ya kwanza itajumuisha Kata 5 zinazokadiriwa kuwa na takribani watu 34,000. |
| **Ushirikiano wa Luswisi** | Kwenye eneo la Luswisi, Kampuni ya Ensol Ltd. Tanzania inaendeleza Mradi wa nishati ya nguvu za maji ulio chini ya Kampuni ya Bwelui unaotegemewa kuzalisha kiasi cha 4.7MW.<br><br>Awamu ya kwanza itajumuisha Kata 4 zinazokadiriwa kuwa na takribani watu 25,000. |

IWaSP INTERNATIONAL WATER STEWARDSHIP PROGRAMME UKaid giz LAKE NYASA BASIN WATER BOARD LNBWB KIWIRA ENERGY LTD. Ensol Energy with a smile

# Ushirikiano Wa Nishati Endelevu Ya Nguvu Za Maji Kidakio Cha Kiwira

### *Muhtasari wa shughuli*


Shughuli za msingi kwenye ushirikiano huu zimegawanywa katika **maeneo 6 ya kufanyia kazi**.

Eneo la kwanza linalenga **kukusanya na kubadilishana taarifa na data** kati ya Bonde la Ziwa Nyasa na wadau. Hii inajumuisha msaada wa kiufundi ili kuanzisha mifumo data ya kijiografia ambayo itatumiwa kwa ajili ya mipango mbalimbali katika Bonde la Ziwa la Nyasa; kupitia mifumo iliyopo na kusaidia kuanzisha, kuthibitisha na kuchambua data za mifumo ya maji kwenye vidakio vyenye upungufu.

Eneo la **uongozi na upangaji wa rasilimali za maji** unalenga kuimarisha ufuatiliaji wa watumia maji, kufanya ukaguzi wa vibali na utaratibu maalumu wa usimamizi na ufuatiliaji. Eneo hili litachukua maarifa yaliyotokana na kazi kama hii iliyofanyika katika Bonde la Pangani.

Ushirikiano huu umeandaa pia shughuli mbalimbali pia zinazolenga kusaidia juhudi za uanzishwaji wa jumuiya za watumia maji ili kuhakikisha **ushirikishwaji madhubuti wa wadau** katika upangaji na kufanya maamuzi.

Katika eneo la **uhifadhi** wa kidakio cha Kiwira, kazi zilizomo ni pamoja na kufanya tafiti ili kufahamu hali halisi ya kidakio na kubainisha maeneo ambayo yanahitaji hatua za haraka za kuyahifadhi. Utaratibu madhubuti utawekwa ili kuhakikisha wa ufuatiliaji wa kila shughuli kama vile uboreshaji wa mbinu za kilimo endelevu.




Eneo la tano la mpango kazi linalenga kutoa msaada wa kitaalamu katika **uendelezaji wa miradi ya nishati ya nguvu za maji**, ikiwa ni pamoja na kusaidia mchakato mzima wa ushirikishwaji wa wadau na wananchi, kutumika kanuni za matumizi endelevu ya rasilimali maji kuanzia kubuni, utekelezaji na uendeshaji wa miradi mbalimbali ya nishati itokanayo na nguvu za maji.

Eneo la sita la mpango kazi linahusu **uendeshaji wa mradi** na Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa katika kuongoza mradi na IWaSP ikisaidia kuongoza na ufanyaji kazi wa pamoja baina ya wadau.



Mto Kiwira, August 2017

### *Matokeo na Manufaa ya Ushirikiano*

| Matokeo | Manufaa yanayotarajiwa |
|---|---|
| Uanzishwaji wa misingi bora na taratibu za utumiaji wa maji | Upatikanaji wa taarifa na data muhimu zanazohusu maji miongoni mwa wadau na Bodi ya Bonde la Ziwa nyasa |
| Jumuiya moja ya watumia maji imeanzishwa | Mawasililiano yaliyoimarika miongoni mwa wadauna ushirikishwaji. |
| Mazingira bora kwa ajili ya shughuli za uzalishaji umeme wa nguvu za maji yametayarishwa | Uhifadhi bora wa mazingira na mito |

**Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na:**

Fridtjof Behnsen
Mratibu wa IWaSP Tanzania
Fridtjof.Behnsen@giz.de
www.iwasp.org
www.giz.de

Tumaini Mwaijega
Afisa Maendeo ya Jamii – Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa
+255 754 083 390
Tumaini.mwaijega@maji.go.tz
www.lakenyasabasin.com

Chapisho hili limeandaliwa na International Water Stewardship Programme (IWaSP): Hata hivyo,linaonyesha mitazamo wa waandishi tu, na wala si IWaSP, wala wafadhili wake BMZ na DfID wala sio watekelezaji wake GIZ wanaweza kuwajibishwa kwa matumizi yeyote ya taarifa yeyote iliyopo kwenye chapisho hili.